**JESMA 001**

# JARIBIO LA KWANZA K.C.P.E
## DARASA LA NANE 2021

**KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - I pekee.
A. kahawa, fedha;
B. chumvi, chupa
C. sukari, mvua
D. mali, chai

Jibu sahihi ni C

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 A B C D | 11 A B ▬ D | 21 A B C D | 31 A B C D | 41 A B C D |

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Umuhimu wa teknolojia ya kisasa ___1___ maisha ya binadamu ___2___ kupuuzwa ___3___. ___4___ sekta zilizonufaika pakubwa ___5___ na uvumbuzi huu ni ile ya mawasiliano. Hapo zamani mawasiliano ___6___ katika matumizi ya mbinu kama vile ___7___ upigaji wa magoma, kuwasha moto ___8___ moshi angani ___9___ kuwatuma wajumbe mbalimbali.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. ya | B. wa | C. katika | D. kwa |
| **2.** | A. hauwezi | B. huwezi | C. haiwezi | D. hayawezi |
| **3.** | A. kabisa | B. tena | C. vile | D. kamwe |
| **4.** | A. Baadhi ya | B. Kati ya | C. Miongoni ya | D. Mithili ya |
| **5.** | A. kutokana na | B. kulingana na | C. mintaarafu ya | D. zaidi ya |
| **6.** | A. yalikuwa yamejikita | B. yangekuwa yalijikita | C. yamekuwa yakajikita | D. yanakuwa yamejikita |
| **7.** | A. ; | B. _ | C. : | D. --- |
| **8.** | A. uliovusha | B. iliyovusha | C. uliyofusha | D. uliofusha |
| **9.** | A. japo | B. halikadhalika | C. angaa | D. wala |

Shama ___10___ wazo la kujiunga na chuo cha kiufundi kuwa ___11___ kwani ___12___ nafasi ya kujiendeleza maishani. Hata hivyo, alielewa dhahiri shahiri kuwa ___13___ ; yaani ufanisi ___14___ usingepatikana vivi hivi tu bali bidii na uwajibikaji ___15___ ulihitajika.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. aliiona | B. aliuona | C. alijiona | D. aliliona |
| **11.** | A. nzuri | B. njema | C. lema | D. zuri |
| **12.** | A. lingempa | B. linampa | C. litampa | D. limempa |
| **13.** | A. jogoo la shamba haliwiki mjini | B. mtaka cha mvungui sharti ainame | C. mchuma janga hula na wa kwao | D. juhudi si pato |
| **14.** | A. wake | B. wako | C. wenu | D. wao |
| **15.** | A. wenye | B. hiyo | C. wenyewe | D. ambao |

*Kuanzia nambari* **16** *mpaka* **30**, *jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Kiambishi ki- kimetumika vipi katika sentensi ifuatayo.
Wanafunzi wale walikuwa wakizingatia nidhamu.
A. Kuonyesha masharti.
B. Kuonyesha hali ya kuendelea.
C. Kuonyesha jinsi ya kutenda.
D. Kuonyesha vitendo vinavyofanyika pamoja.

**17.** Kutokana na kitenzi **vumilia** tunapata sifa gani?
A. Uvumilivu
B. Kuvumilia
C. Vuma
D. Vumilivu

**18.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
Sonara alinifulia mkufu huu.
A. Sonara walitufulia mikufu hii.
B. Masonara walinifulia mikufu hii.
C. Sonara walitufulia mikufu hizi.
D. Masonara walitufulia mikufu hii.

**19.** Ipi ni sauti ghuna?
A. b
B. th
C. sh
D. f

**20.** Chagua ukanushaji wa sentensi ifuatayo.
Bakari ameuchukua mkoba wake.
A. Bakari hakuuchukua mkoba wake.
B. Bakari hajauchukua mkoba wake.
C. Bakari hauchukui mkoba wake.
D. Bakari hatauchukua mkoba wake.

**21.** ____ ni mtu ambaye huwabebea watu mizigo kwa malipo.
A. Dalali
B. Mzegazega
C. Mjumu
D. Hamali

**22.** Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo.
Nyumba **yenu** imejengwa **vizuri** **lakini** **ile** si thabiti.
A. kivumishi, kivumishi, kielezi
B. kiwakilishi, kiunganishi, kiashiria
C. kivumishi, kiunganishi, kiwakilishi
D. kielezi, kiunganishi, kiwakilishi

**23.** Mtu anapotaka kupishwa njia husemaje?
A. Simile
B. Ashakum
C. Samahani
D. Hebu

**24.** Akisami $\frac{5}{7}$ kwa maneno ni
A. subui tano
B. humusi saba
C. thumni tano
D. saba kwa tano

**25.** Chagua jozi ambayo **hailingani**.
A. simba, shibli
B. nzige, kimatu
C. papa, kinengwe
D. sungura, kinyemere

**26.** Andika kauli ya kutendewa ya sentensi ifuatayo.
Fundi alimshonea Shama kiatu kibandani.
A. Kiatu cha Shama kilishonwa na fundi kibandani.
B. Shama alishonewa kiatu kibandani na fundi.
C. Kiatu kilishonewa kibandani kwa Shama na fundi.
D. Fundi alimshoneshea Shama kiatu kibandani.

**27.** Tegua kitendawili kifuatacho; Hausimiki hausimami.
A. Moto
B. Mkoba
C. Moshi
D. Mkufu

**28.** Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.

A. Kibe ni kijana mpole: Yeye ni mwerevu darasani.

B. "Uwanja huu, " akasema mwalimu una nyasi ndefu.

C. Wakazi - wengi wa mtaa huu - ni wafanyabiashara.

D. Selina (yule wa runingani) ana sifa kochokocho.

**29.** Kanda ni utepe wa kunasia sauti au picha. Kanda pia ni

A. mfuko wa ngozi wa kuhifadhia vitu.

B. namna ya chombo cha usafiri baharini.

C. mtu mwenye tabia ya udanganyifu.

D. kuivisha vitu kama mikate kwenye joko.

**30.** Andika methali yenye maana sawa na hii.
**Kikulacho ki nguoni mwako.**

A. Ibilisi wa mtu ni mtu.

B. Mla nawe hafi nawe ila nızaliwa nawe.

C. Zimwi likujualo halikuli likakumaliza.

D. Dawa ya moto ni moto.

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40**

Mwili wa mwanadamu hauwezi kufanya kazi kama inayotarajiwa iwapo hauna afya. Watu wengine hudhani kuwa afya ni jambo la nasibu tu. Hawa huachilia miili yao kufanya kazi kama punda bila kujali maslahi yao. Mtu asiyejali rai yake huchakaa haraka na kuwa dhaifu.

Njia mojawapo ya kuhakikisha kuwa mwili una nguvu na siha inayostahili ni kupitia kwa vyakula. Uzingatiaji wa lishe bora ni muhimu kwa afya ya mwanadamu. Lishe bora **huurutubisha** mwili na kuuacha ukiwa katika hali nzuri. Maandalizi bora ya vyakula ni kuhakikisha kuwa vimeiva kabisa ili kuepuka maumivu ya tumbo na kasoro nyinginezo. Aidha, vyakula visivyoandaliwa vizuri humfedhesha mwenyeji mbele ya wageni wake.

Ulaji wa chakula haumaanishi kula bila breki. La, unamaanisha kula vyakula ambavyo vina manufaa kwa mwiili yetu. Baadhi ya watu hula vyakula vyenye wingi wa mafuta. Mafuta mengi hatimaye huleta madhara hasa kwa mtu asiyefanya mazoezi ya viungo vya mwili. Ulaji wa mayai kwa wingi pamoja na nyama ya kuchoma huweza kumletea mlaji matatizo ya kiafya. Vyakula hivi na vingine huhitaji kuliwa kwa vipimo.

Mikono haina budi kuwa safi kabla ya kuanza kula. **Kwa wengine, kunawa ni kaida tu**; hawatumii sabuni kamwe. Kukipakia chakula bila kuzingatia usafi huweza kusababisha uele wa waba. Isitoshe, maji yasipochemshwa huweza kusababisha maradhi haya. Ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha kuwa viwango vya usafi vimezingatiwa kila wanapotaka kula.

Yapo maradhi mengine ambayo husababishwa na wadudu. Mfano wa haya ni malaria na malale. Ni vyema kuzingatia usafi wa mazingira yetu ili kuyaepuka magonjwa haya. Vitu vinavyovunda navyo visiachwe kuzagaa kila mahali ili kuwaondoa nzi wanaoweza kueneza magonjwa. Aidha, nyasi na vichaka vinafaa kufyekwa bila kusahau kuondoa mikebe na vidimbwi vya maji taka.

Uvutaji wa sigara na ulevi ni baadhi ya tabia ambazo huwaletea waja matatizo ya kiafya. Moshi unaovutwa una madhara mengi sio tu kwa afya ya mvutaji bali pia kwa walio karibu naye. Pombe humdhuru mnywaji kwa namna nyingi ; kuna wale ambao hukumbwa na tatizo la ini. Miili ya hawa hushindwa kufanya kazi na hivyo wakaishia kutangulia mbele ya haki.

Mwili vilevile huhitaji mazoezi ya viungo ili kuweza kubaki katika hali nzuri ya afya na utendakazi. Baadhi ya watu hufanya mazoezi ya kukimbia asubuhi na jioni jioni. Wengine hutembea masafa fulani ili kama wanavyosema wenyewe kunyosha miguu. Wengi hununua baiskeli ili watumie nguvu kuziendesha; kusudi damu ipate kuranda vizuri kote mwilini na viungo kunyooka. Baadhi hujinunulia vifaa vya kufanyia mazoezi nyumbani au kulipa ada ya kutumia sehemu zenye vifaa hivyo.

Rai zetu ni ngao zetu. Bila siha, sisi silolote si chochote. Mtu huwa kama gogo tu. Ni wajibu wetu kuzingatia na kufanya yote tunayoweza ili kuhakikisha kuwa siha zetu hazituponyoki.

**31.** Chagua maelezo sahihi kulingana na aya ya kwanza.
A. Mwili wa mwanadamu haufanyi kazi yoyote bila afya.
B. Afya ya mwanadamu ni jambo la nasibu.
C. Afya huusaidia mwili kuendesha shughuli ipasavyo.
D. Mwili wa mwanadamu unapochakaa madhara ya afya nzuri hujulikana.

**32.** Kwa nini vyakula visipoivishwa vizuri huleta hasara?
A. Vyakula hivyo hukosa virutubishi.
B. Vyakula hivi haviwezi kutafunika.
C. Mwili hushindwa kuondoa vyakula hivi.
D. Husababisha shida za afya na kuleta aibu.

**33.** Ulaji mzuri ni ule wa
A. kutumia vipimo vidogo vya chakula.
B. kutumia kipimo kikubwa cha vyakula.
C. kutumia kipimo kifaacho cha chakula.
D. kutumia kipimo chochote cha chakula.

**34.** Kuhusu vyakula vya mafuta, mwandishi wa makala haya anapendekeza kuwa,
A. wanaotumia mafuta mengi wafanye mazoezi.
B. watu wasitumie mafuta katika vyakula.
C. vyakula vyenye mafuta vitumiwe na watu wenye miili midogo.
D. viliwe kwa wingi ili kuimarisha afya ipasavyo.

**35.** **'Kwa baadhi, kunawa in kaida tu'** kauli hii ina maana gani?
A. Watu wote hunawa vizuri kabla ya kula.
B. Wengine hunawa kimazoea tu bila kuwa makini.
C. Wengine hunawa kwa kulazimishwa tu.
D. Wao hunawa kwa njia ifaayo wakati wote.

**36.** Mdudu anayeambukiza ugonjwa wa malale huitwaje?
A. Mbung'o
B. Mbu
C. Parare
D. Funza

**37.** Sigara huwa na madhara yapi?
A. Kuwaathiri hata walio mbali sana na mvutaji.
B. Humwathiri mvutaji peke yake.
C. Huwaathiri wengine badala ya mvutaji.
D. Humwathiri mvutaji na walio karibu naye.

**38.** Watu hununua baiskeli kwa sababu.
A. kuimarisha afya zao.
B. kufika kazini haraka.
C. kuwabebea jamaa zao.
D. kumaliza nguvu zao.

**39.** Kulingana na aya ya mwisho,
A. mtu asipokuwa na afya hugeuka kuwa gogo.
B. afya ni silaha ya kujikinga na maadui.
C. ni vyema kuzingatia njia mbalimbali za kuboresha afya.
D. ni vizuri watu wanene watembee kuimarisha afya.

**40.** Maana ya neno **'huurutubisha'** jinsi lilivyotumika ni
A. huunenepesha
B. huustawisha
C. hudhalilisha
D. huutia mbolea

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali kuanzia* **41** *mpaka* **50**

Juma alipiga goti huku machozi yakimdondoka njia nne nne. Mbele yake palikuwa na makaburi mawili. Waliokuwa wamelala mle hawakuwa na habari juu ya kihoro na simanzi ya aliyepiga magoti pale. Lala kwanza lilikuwa kongwe kiasi na lilikuwa limemea vichaka na magugu. La pili lilionyesha upya kwani mashada ya maua yaliyowekwa na waombolezaji yalikuwa bado mabichi. Babake na mamake Juma walikuwa wamelazwa makaburini humu mtawalia.

Kwa Juma, maisha hayakuwa na maana tena. Alikuwa mwanafunzi wa miaka kumi na miwili na alikuwa katika darasa la saba. Hakuwa amchitimu kujitegemea na kukimu mahitaji yake. Aliokuwa akiwategemea sasa wamemwacha akiwa yatima. Hakuna yeyote ambaye angelijaza pengo lililo achwa na wavyele wake. Zaidi ya haya alisononeka kuwapoteza wazazi wote wawili kwa kipindi cha miaka miwili tu. Haya yalikuwa kwake kama dondandugu lisilopona.

Kwa sasa Juma anayakumbuka mengi. Anakumbuka maisha ya babake. Alikuwa jibaba zito na lenye sura jamala na siha nzuri. Baba mtu alikuwa na chake na alijiweza kiuchumi. Wengi pale mjini walimheshimu na kumstahi kutokana na uwezo wake huo. Aidha, alitunza familia yake vilivyo. Juma hakumbuki hata siku moja aliyokosa chochote alichohitaji kutoka kwa babake. Alikuwa mwenye bidii kazini mwake pia.

Walakini, kama mja asiyekamilika, baba mtu alikuwa na taksiri moja. Aliyapenda maisha ya anasa na kufukuzia wasichana wadogo mle mjini. Mamake Juma aliyajua fika haya. Alijaribu kuzozana naye ili aache tabia hii potovu. Lakini kila alipothubutu, mama mtu alifokewa na kukemewa kuwa aache upuuzi wa wanawake. Akafika kufyata ulimi na kumwachia Mola ayaongoze maisha ya mumewe.

Hata hivyo, hakuna marefu yasiyo na kikomo. Baada ya kuponda raha na vimanda si haba, alianza kuugua. Maradhi yake yakawa na msururu. Mara alipata mafua yasiyopona, mara kuendesha, mara maradhi ya ngozi. Haya yalimtia wasiwasi. Baada ya kukaguliwa na matabibu kadhaa alipatikana kuwa **"ameumwa na mdudu"** Hakuyaamini haya. Baba aliyekuwa na bashasha na mcheshi aliingiwa na upweke na kutotaka kutangamana na yeyote hata jamaa yake.

Waliosema kuwa hakuna msiba usiokuwa na mwenzake hawakutupaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Maradhi haya yaliifilisi jamaa huku aing'ang'aniwa kupata tiba. Wakaenda kwa waganga na waganguzi. Waganga nao wakafid. tamu.

Muda si muda, mama naye akaanza kuugua. Baada ya uchunguzi akapatikana na ugonjwa sawa na wa bwanake. Ikawa ni kama mji umerogwa. Baadaye babaye akaaga dunia na mamaye hakukawia sana. Akasalimu amri na kumfuata mumewe. Juma, kijana mdogo, akaachwa na upweke.

Kama kawaida, mja hakosi neno. Wengi walisikika wakisema hili na lile kuhusu vifo hivi. Wengine walieneza minong'ono. Lakini Juma alijua ukweli wa vifo vya wazazi wake.

**41.** Juma alipiga goti kwa sababu ya,
A. makaburi yaliyokuwa yamemea vichaka.
B. wazazi wale walikuwa makaburini.
C. huzuni ya kufiwa na wazazi wote.
D. kuweko kwa makaburi mawili.

**42.** Ni kweli kuwa,
A. mama alitangulia kufariki.
B. baba alitangulia kufariki.
C. wazazi walifariki wakati mmoja.
D. baba na mama walifariki baada ya mwaka.

**43.** Babake Juma aliheshimiwa kwa kuwa,
A. alikuwa mwenye sura ya kuvutia.
B. alitunza familia yake vilivyo.
C. alikuwa tajiri wa kutajika.
D. alikuwa mwenye bidii kazini.

**44.** Neno jingine lenye maana sawa na **taksiri** ni
A. dosari
B. huzuni
C. raha
D. fujo

**45.** Chagua sifa za babake Juma kulingana na kifungu.
A. mpenda raha, asiyejali familia yake.
B. mwenye mali, anayejali maslahi ya wote.
C. mwenye sura nzuri, asiyewajibika kazini.
D. mpenda anasa, anayetunza aila yake.

**46.** Baba Juma alimfokea mkewe kwa kuwa,
A. mke alikuwa akifuata uvumi.
B. mke alikuwa akimwambia ukweli.
C. mke alikuwa akimfuatafuata mjini.
D. mke alitaka ushauri kutoka kwake.

**47.** Maana ya kifungu **'amcumwa na dudu'** ni
A. Aliambukizwa maradhi ya UKIMWI.
B. Aliambukizwa maradhi ya kuendesha.
C. Alifikiwa na wadudu ambao walimwuma.
D. Alichokoza wadudu akapata maradhi.

**48.** Methali **'Hakuna msiba usiokuwa na mwenzake'** inamaanisha,
A. kumliwaza mgonjwa kulileta huzuni.
B. familia ya mhusika iliambukizwa maradhi ya baba.
C. kuugua kwa mama kulimletea baba huzuni.
D. ugonjwa wa mzazi ulifuatwa na matatizo mengine.

**49.** Maelezo yapi **si** sahihi kulingana na kifungu?
A. Juma hakuelewa chanzo cha vifo vya wazazi.
B. Majirani walijua chanzo cha vifo vya wazazi.
C. Mgonjwa alipotibiwa hakupata nafuu.
D. Baba alipofariki mama hakuishi muda mrefu.

**50.** Funzo la kifungu hiki ni kuwa,
A. Kufuata starehe sana hakuna mwisho mwema.
B. Mara nyingi UKIMWI huambukizwa wale wanaojitunza vyema.
C. Kubaki yatima kulimfanya Juma awajali wazazi.
D. Kuambukizwa maradhi huileta familia pamoja.